



KARIBU UWEKEZE
KATIKA HALMASHAURI
YA WILAYA YA MLELE

Tunatekeleza

www.mleledc.go.tz

HALMASHAURI YA WILAYA

MLELE



TAREHE 9 FEBRUARI 2021

**UTEKELEZAJI WA MAAGIZO YA MHE. SELEMANI JAFU WAZIRI WA NCHI OR - TAMISEMI
KWA WATENDAJI WA HALMASHAURI YA WILAYA YA MLELE**



Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mlele Mwl Alexius Revocatus Kagunze akitoa maagizo ya Mhe, Waziri wa Nchi OR TAMISEMI Mhe, Selemani Jafo kwa Watendaji wa Halmashauri ya wilaya ya mlele wakati wa Kikao cha Watendaji wa Halmashauri kilichofanyika ukumbi wa Maktaba Shule ya Sekondari Inyonga, kulia kwa Mkurugenzi ni Katibu Tawala wa Wilaya ya Mlele Mhe, Linkolin Tamba.



Mwendaji wa Kijiji cha Ipwaga akisoma maagizo kwa kauli yake mwenyewe baada ya kuambiwa na mkurugenzi awasomee watendaji wenzake kuonesha msisitizo baada ya kupewa na Mkurugenzi Mtendaji kuonesha msisitiza kuwa atatekeleza kama alivyoelekezwa, huku watendaji wenzake wakisikiliza kwa umakini kama inavyoonekana pichani.



Katibu Tawala wa Wilaya ya Mlele Linkolin Tamba akisisitiza Jambo kwenye Maagizo yaliyotolewa na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri aliyekaa kushoto kwake baada ya kuwapa maagizo watendaji wa Halmashauri hawapo pichani kuonesha namna maagizo hayo yalivyo muhimu



Watendaji wa Halmashauri wakipokea maagizo ya Mhe, Waziri wa Nchi OR - TAMISEMI Mhe, Selemani Jafo, aliyoyatoa kwa Wakurugenzi na Makatibu Tawala wote tarehe 3/2/2021 na kuwataka wakurugenzi hao kuyashusha kwa watendaji wao.

Imeandaliwa na Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya ya Mlele



Mtendaji wa Kijiji cha Kaulolo Mr Jackson Shula akipokea Zawadi ya Kitambaa cha Suti kutoka kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Mlele kwa kutambua utendaji wake wa Kazi.



Watendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mlele wakiwemo wakuu wa Idara na Vitengo na Afisa Tarafa Inyonga wakimsikiliza Mkurugenzi Mtendaji, akiwapa maagizo watendaji hao yaliyotoka kwa Mhe, Waziri wa Nchi Ofisi Rais (TAMISEMI) Mhe, Seleman Jafo, aliyoyotoa kwa Wakurugenzi na Makatibu Tawala wote siku tarehe 3/2/2021.



Baadhi ya Wakuu wa Idara na Vitengo wakiongozwa na Afisa Utumishi na Utawala Samson Meda mwenye shati la kijivu, Mganga Mkuu wa Halmashauri, mwenye shati jeupe Kaimu Afisa Maendeleo ya Jamii na Mwisho ni Mkuu wa Idara ya Fedha Obindi Jeremia Wembe mwenye Shati Jekundu wakimsikiliza maagizo kutoka kwa Waziri wa Nchi OR TAMISEM Mhe Seleman Jafo yaliyotolewa na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mlele Hayupo Pichani.

MAAGIZO YA KIKAO NI PAMOJA NA:

1. Ukusanyaji wa Mapato kutoka kwenye majengo ambapo wametakiwa kuwa na orodha ya nyumba zote zilizoko kwenye maeneo yao nyumba za bati zilipiwe kodi.
2. Wahakikishe wanatoza ushuru wa Mabango.
3. Kuhakikisha Vitambulisho vya wajasiliamali wanapatiwa wajasiliamali wote wenye sifa za kuwa wajasiliamali wadogo.
4. Wenyeviti wa Vijiji na watendaji waitishe mikutano ya vijiji na vikao vya kisheria vifanyike kwa maendeleo ya kijiji
5. Kutatua kero za wananchi vijijini kwa wakati
6. Kuhamasisha maendeleo vijijini, kwa kuhamasisha wananchi wajitolee
7. Kila mmoja atimize wajibu wake.
9. Waboreshe uchumi shindani



**KARIBU UWEKEZE KATIKA HALMASHAURI
YA WILAYA YA MLELE. PAMOJA
TUNATEKELEZA 2021**

Imeandaliwa na Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya ya Mlele